Jukumu la Meiji Gakuin katika vita na baada ya vita:

Toba

Mbele yako Mwenyezi Mungu, tukiadhimisha miaka hamsini tangu kushindwa kwa Japan kwenye vita, natubu dhambi ya Meiji Gakuin iliyoitenda katika hiyo vita, na ninakiri makosa yetu dhidi ya Wakorea, Wachina na dhidi ya mataifa mengine.

Tunapokaribia kuadhimisha miaka hamsini tangu kushindwa kwa Japan, uhasama wa vita hiyo unaendelea kubainika waziwazi na katu hatuwezi sahau. Madhara ya vita; janga lililowapata wanawake waliotumiwa kuwaburudisha wapiganaji, upasuaji uliofanywa kwa akina mama na kikundi cha ‘731’ cha majaribio ya Bayo-Kemia; hivi ni vidonda ambavyo bado vyakithiri; manusura na familia zao bado wanaumia siku baada ya siku.

Mataifa mengi yaliadhirika na uhasama wa Wajapani katika vita hiyo. Ingawaje vita ilikuwepo Japan, Meiji Gakuin haikukosa kujihusisha nayo, ingawa msingi wa vita ulikuwa jina na upendo wa Yesu.

Ingawaje ni wazi kwamba shule za kibinafsi hazikuwa na msimamo mathubuti kuhusu mamlaka ya taifa, Meiji Gakuin ilidumisha, azma ya waanzilishi, wa ‘Ukristo kama msingi wa elimu wakati historia yote yake inayojulikana. Lakini, mbele ya Bwana wetu Yesu Kristo, hatuna sababu ya huzuni ambayo Meiji Gakuin hubeba kwa kuhusika na vita hiyo ya uvamizi. Hakika sisi vizazi vya baadaye ambao hatukushuhudia magumu ya wakati huo, hatuna haki ya kuwalaumu viongozi wa nyakati hizo za vita. Haki ni kwa Mwenyezi Mungu kuwahukumu wao na mashirika yao. Lakini tunayo nafasi ya kuelewa kwa upana na urefu madhara ya vita kupitia ushuhuda ambao unazidi kuongezeka kutoka kwa waadhirika wa uvamizi, dhuluma, na kutoka kwa waliopeana maisha yao kwa haki ya Kristo. Ili kwamba tuwe katika nafasi nzuri katika kuuchambua vyema kuliko viongozi wa nyakati hizo. Hivyo basi, ni lazima tuyatubu makosa ya hao viongozi mbele ya Mwenyezi Mungu na tukiri makosa yetu dhidi ya waadhirika. Maana ya kufanya hivi si kuwaadhibu hao viongozi ila nikuhakikisha kwamba sisi wenyewe hatuta tenda makosa kama haya.

Kufuatia Tukio la Manchuria la 1931 na kutokea kwa vita baina ya Uchina na Japan mwaka wa 1937, serikali ilipitisha Sheria ya Mashirika ya Dini mwaka wa 1939, na kwa msingi huo wakaanza kanisa la United Church of Christ Japan(UCCJ-Nihon Kirisuto Kyodan) mwezi wa sita, mwaka wa 1941, ili

kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano baina ya makundi ya kidini na kanuni za serikali. Kasisi Mitsuru Tomita mwenyewe, mkuu wa UCCJ (Tori), alizuru mahali patakatifu pa Ise Shinto na akawafanya Wakristo wa Korea wazuru mahali hapo mwaka wa 1938. Hakuna shaka kwamba kitendo hiki kilisababisha Wakristo wengi Wakorea kujipeana, na kusababisha mgawanyiko mkubwa kati ya Wakristo wa Japan na Korea. Shule nyingi za misheni za Korea na Taiwan zilikumbwa na shida za kuabudu mahali patakatifu. Tomita alikuwa mwenyekiti wa kamati la wasimamizi wa Meiji Gakuin kwa miaka mingi, kabla na baada ya vita.

Tsuraki Yano, aliyekuja kuwa Mkuu wa Meiji Gakuin mwaka wa 1939 alikuwa muunga mikono wa vitendo kama kuinama upande wa ikulu ya wabeberu, kutembelea mahali patakatifu pa Yasukuni, na utiifu mbele ya chongo la ubeberu. Bila kutubu dhambi zake kwa Mola, alibaki kwenye kiti cha utawala kwa muda mrefu baada ya vita. Meiji Gakuin haikuwahi hadi ya leo, kutubu haya maovu mbele ya umma kwa Mola au kuyakubali makosa yaliyofanyika kwa watu wa nchi ambazo zilivamiwa na Japan. Tomita na wengine walikuwa kwenye viti vya uongozi katika kanisa la UCCJ wakati kanisa hilo lilipoitisha misaada ya kukumbana na ndege chini ya andishi la ‘*Peperusha!* Ndege ya UCCJ’ na pia wakati gazeti lake la Kyodan Jiho lilipowaomba Wakristo kutii uongozi wa mbeberu likisema kwamba ‘kujipeana kwa niaba ya nchi ni kama kufa ukilinda

jina la Mola**.** Hata tukichukulia uongozi wa nguvu uliokuweko wakati huo, na upiganiaji wa haki za kanisa hatuwezi kukataa kwamba tulihusika na maovu yaliyotendwa na nchi ya Japan, uongozi ulioleta matatizo yaliyotajwa hapo awali. Ninapofikiri juu ya wanafunzi waliotumwa kupigana katika mazingira haya na kuhusika na vita vya uvamiaji, siwezi kujizuia kusikia uchungu kama mwalimu na mkuu wa chuo hiki. Hili jambo pia linanipa ufumbuzi juu ya walimu wa wakati wa vita ambao waliwatuma vijana wengi kuwa mstari wa mbele wakiwemo wanafunzi kutoka Korea na Taiwan. Kwa uhakika, viongozi wa Chuo hiki wangefikiria juu ya vitendo vyao watubu dhambi zao na wakubali makosa yao baada ya kushindwa kwa vita ya Wajapan wakati Mweyezi Mungu atakapotuonyesha hukumu yake.

Hakukuwa na tangazo la umma la kuomba msamaha kamwe baada ya vita. Badala yake, fikira la kuomba roho za Wajapani ambao walikufa katika vita ya chuki halikuoponyoka Meiji Gakuin.

Joji Tagami, ambaye alikuwa ni mwanakamati wa kundi la uongozi ambaye jukumu lake lilikuwa ni kulinda azma ya waanzilishi wa Meiji Gakuin, alishauri serikali ijiunge na juhudi za kuzuru pahali pa mashujaa wa vita. Hii ni thibitisho kwamba, hata baada ya vita, Meiji Gakuin iliendelea kujihuzisha na uhasama ule

ule alioutenda Tomita katika vita, yaani kuabudu wafu kama miungu, uabudu wa sanamu ambayo ni dhambi inayomchukiza sana Mwenyezi Mungu, aliyejifunua kwetu katika Biblia.

Kwa hivyo swala la jukumu la vita hii inahusika moja kwa moja na toba ya matendo ya kivita. Bila ya kuyatatua maswala haya, Meiji Gakuin haitaweza kuipata njia ya ufanisi wa siku za baadaye.

Lakini tunapoangalia historia ya vita ya Meiji Gakuin leo, miaka hamsini baada ya kushindwa kwa Japan, tunaweza kuona mwangaza wa tumaini kwamba kulikuwa na wanafunzi wenye hisia njema kama Shin Hasegawa. Uchungu wake kwa kutumwa kwenye vita na roho yake ya uhuru wa kindani kutoka kwa serikali ya wabeberu inatoa maoni kwamba, Meiji Gakuin, katika siku za usoni, inapaswa kufuata mafundisho ya Yesu Kristo pekee. Ningetaka kuamini kwamba kuna baadhi ya wanafunzi wengine waliopambana kuishi maisha yao kama Shin.

Tunapoelekea karne ya ishirini na moja; na kuitikia upya azimio la waanzilishi, ni lazima Meiji Gakuin iende mbele sio kwa ile ‘njia pana’ walioifuata Tomita, Yano na wengineo. Badala yake, waifuate ile nyembamba alioifuata Hasegawa, ambaye alikuwa mwanafunzi wakati huo. Fikira ya ‘sadaka kwa

taifa’ inapoendelea kusambaa tena katika jamii ya Wajapani, na vile Japan inaanza kutuma majeshi kwenye mataifa ya nje kwa jina la ‘mchango wa kimataifa’, siwezi kujizuia kuhisi adhari kwamba wafu wataabudiwa tena kama miungu, kwa jina la mashujaa wa vita. Kwanza lazima tufikirie kwa undani kuhusu jukumu la hiki chuo wakati na baada ya vita. Tufanye toba mbele ya Bwana Wetu Yesu Kristo, na ijulishwe kwa umma. Kwa kuitikia makosa yetu dhidi ya watu ambao mataifa yao yalivutwa kwenye vita hii, tunaweza kuwa na njia za kutatua vita hii kwa ukamilifu, ndivyo tuweze kuwa bila lawama. Wana wa Mungu wasio na kosa kati ya kizazi kisicho na mwelekeo, kati yao tuangaze kama nyota ulimwenguni. (Waphilipi 2:15).

Tunatoa toba kwa Mwenyezi Mungu na tunaonyesha unyenyekevu kwa walioadhirika na vita ili Meiji Gakuin ieneze imani ya kweli katika Yesu Kristo.

Hiromasa Nakayama

Chancellor wa Meiji Gakuin

Azimisho la tano tangu kushindwa kwa Japan katika Vita ya Pili ya Dunia

Juni 1995